



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WATAHINIWA WA UALIMU CHETI DARAJA
LA III A (GATCE) 2022**

STADI ZA KAZI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WATAHINIWA WA UALIMU CHETI DARAJA LA III
A (GATCE) 2022**

634 STADI ZA KAZI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2022

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI	IV
1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI	2
2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI	2
2.1.1 Swali la 1: Maandalizi ya Ufundishaji.....	2
2.1.2 Swali la 2: Ushonaji wa Nguo	4
2.1.3 Swali la 3: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi	7
2.1.4 Swali la 4: Biashara Ndogo Ndogo	9
2.1.5 Swali la 5: Ufundishaji	12
2.1.6 Swali la 6: Udobi	15
2.1.7 Swali la 7: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi	18
2.1.8 Swali la 8: Sanaa za Maonesho	22
2.1.9 Swali la 9: Muziki	24
2.1.10 Swali la 10: Sanaa za Maonesho	27
2.2 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA.....	29
2.2.1 Swali la 11: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi	30
2.2.2 Swali la 12: Upishi	34
2.2.3 Swali la 13: Ufundishaji	39
2.2.4 Swali la 14: Upimaji.....	42
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA.....	48
4.0 HITIMISHO	48
5.0 MAPENDEKEZO	49
KIAMBATISHO	50

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitim Mafunzo ya Ualimu Daraja la A kwa somo la Stadi za Kazi. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanachuo, wakufunzi, waandaa sera, wadau wa elimu na jamii kwa ujumla jinsi watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani.

Taarifa hii ni tathmini ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi. Kimsingi, majibu ya watahiniwa katika maswali ya mtihani ni uthibitisho wa yale ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa katika mafunzo ya Ualimu katika daraja hili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri au vibaya katika kujibu maswali ya mtihani. Sababu zilizowafanya watahiniwa wengi kumudu kujibu maswali kwa usahihi ni pamoja na kuwa na uelewa mzuri wa mada husika, uwezo wa kujenga hoja na kuelewa matakwa ya swal. Aidha, sababu za watahiniwa wachache kushindwa kupata alama za juu katika baadhi ya maswali ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya maswali, kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana zilizopimwa, kutoa maelezo yasiyojitosheleza na uelewa mdogo katika kujibu maswali ya insha.

Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wathibiti ubora wa elimu, wakufunzi na wanachuo kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kutayarisha taarifa hii.



Athuman S. Amasi
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Stadi za Kazi kwa watahiniwa wa mtihani wa Ualimu Daraja la IIIA uliofanyika Mei 2022, uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Stadi za Kazi wa mwaka 2009 na fomati ya mtihani ya mwaka 2022.

Mtihani huu ulikuwa na jumla ya maswali kumi na nne (14) yaliyogawanywa katika sehemu mbili: A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 ya majibu mafupi kutoka katika mada za taaluma na ufundishaji. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote, sehemu B ilikuwa na maswali manne ya insha kutoka katika mada za taaluma na ufundishaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Mtihani wote ulikuwa na jumla ya alama 100 zilizogawanywa katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na jumla ya alama 40 na kila swali lilikuwa na alama 4, wakati sehemu B ilikuwa na jumla ya alama 60 na kila swali lilikuwa na alama 15.

Ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa somo la Stadi za Kazi kwa mwaka 2022 ulikuwa mzuri. Jumla ya watahiniwa 3,251 walifanya mtihani, ambapo wote 3,251 sawa na asilimia 100 walifa kwa kupata alama 40 na zaidi. Kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani asilimia 1.35 walipata daraja A, asilimia 46.35 walipata daraja B, asilimia 51.40 walipata daraja C na asilimia 0.89 walipata daraja D. Aidha, hapakuwa na watahiniwa waliopata daraja F. Kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2022 kimepanda kwa asilimia 0.1 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 99.90.

Ufaulu wa watahiniwa katika taarifa hii umegawanyika katika viwango vitatu ambavyo ni ufaulu mzuri unaoanzia alama 70 hadi 100, wastani unaoanzia alama 40 hadi 69 na hafifu unaoanzia alama 0 hadi 39. Chati za viwango vya ufaulu kwa asilimia zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu wa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Taarifa hii inachambua maswali yenyeye ufaulu mzuri, wastani na hafifu kwa kina ili kuongeza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi. Aidha, taarifa hii inaonesha sababu zilizowafanya watahiniwa kupata ufaulu mzuri, wastani au hafifu katika majibu ya maswali ya baadhi ya mada. Sampuli za majibu ya watahiniwa

zimeambatishwa ili kuonesha kile walichofanya. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi kwa mada ambazo ufaulu ulikuwa hafifu ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani yao. Aidha, inategemewa kuwa matokeo ya uchambuzi huu yatawanufaisha wanachuo, wakufunzi, waandaaji wa sera na wadau wote wa elimu kwa ujumla.

2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu A ilikuwa na maswali ya majibu mafupi kumi (10) kutoka katika mada za taaluma na utaalamu. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na jumla ya alama 4. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu, ambapo kiwango cha ufaulu mzuri kilikuwa ni alama 3.0 hadi 4.0, ufaulu wa wastani alama 2.0 hadi 2.5 na ufaulu hafifu alama 0.0 hadi 1.5.

2.1.1 Swali la 1: Maandalizi ya Ufundishaji

Swali hili liliwataka watahiniwa kutumia maarifa waliyopata katika uchambuzi wa muhtasari wa somo la Stadi za Kazi, kuainisha taarifa nne muhimu zinazopatikana katika ukurasa wa haki miliki. Swali lilijibowi na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa hafifu kwani jumla ya watahiniwa 520 (15.9%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Jedwali Na. 1 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.

Jedwali Na. 1: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia (%)
0.0 – 1.5	2754	84.1
2.0 – 2.5	468	14.3
3.0 – 4.0	52	1.6

N = 3,274

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa, watahiniwa 2,754 (84.1%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 amba ni ufaulu hafifu, watahiniwa 468 (14.3%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 amba ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 52 (1.6%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 amba ni ufaulu mzuri.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 2,754 sawa na asilimia 84.1 waliopata alama kuanzia 0 - 1.5, hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kupelekea kutoa majibu yasiyo sahihi. Baadhi ya watahiniwa waliainisha faida za kutumia muhtasari badala ya taarifa muhimu zilizo katika ukurasa wa haki miliki. Watahiniwa wengine waliainisha maudhui yaliyomo ndani ya muhtasari. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

- (i) *Mada Kuu: Huonesha jambo kuu ambalo litatakiwa kubeba mada ndogo.*
- (ii) *Mada ndogo: Huonesha vipengele mbalimbali kutoka kwenye mada kuu.*
- (iii) *Njia /mbinu za kufundishia: Huonesha namna ya kuwasilisha somo.*
- (iv) *Muda na Matumizi ya Zana: Huonesha wakati unaopaswa kutumia na zana.*

Aidha, watahiniwa wengine waliainisha vipengele vya andalio la somo badala ya taarifa muhimu zilizo katika ukurasa wa haki miliki. Mfano mtahiniwa mmoja aliandika *Umahiri Mkuu, Umahiri Mahsus, Rejea na Darasa*, ambazo sio taarifa muhimu zinazopatikana katika ukurasa wa haki miliki kwenye muhtasari wa somo la Stadi za Kazi. Kadhalika, watahiniwa wengine walichanganywa na neno ‘Haki miliki’ hivyo walitoa hoja kuhusiana na haki za binadamu. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika;

- (i) *Haki za binadamu zifuatwe kisheria*
- (ii) *Kila mtu ana haki ya kumiliki kile kilicho chake bila kudhulumiwa*
- (iii) *Serikali itamchukulia hatua ye yeyote ambaye atakiuka haki za sharia za nchi.*

Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

1	<p>i) Muhtasari kuyardia kujua Mada zote zinazotakiwa kufundishwa kwa Watengwa husika a kwa Nuda Maalumu.</p> <p>ii) Husaidia kujua jinsi Mada zilizopangwa kwa Miririko Ncuri Unaofaa.</p> <p>iii) Husaidia kufanya Upimaji wa aina Moja kwa Wanafunzi wote katika Somo husika.</p> <p>iv) Husaidia kujua Mbini na njia bora za kufundishia somo la Stadi za Kazi Mashuleneni.</p>
---	---

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1.


Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa aliainisha umuhimu wa muhtasari katika ufundishaji badala ya taarifa nne muhimu zinazopatikana katika ukurasa wa haki miliki.

Hali kadhalika, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 520 (15.9%) waliopata alama kuanzia 2 mpaka 4 katika swali hili, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uchambuzi wa muhtasari wa somo la Stadi za Kazi. Baadhi ya watahiniwa waliweza kuainisha taarifa muhimu mbili hadi tatu kati ya nne zilizohitajika katika swali. Watahiniwa wengine walichanganya taarifa muhimu za muhtasari pamoja na hoja zisizo sahihi, hivyo kushindwa kupata alama zote. Hata hivyo, watahiniwa wachache walimudu kuainisha taarifa muhimu zinazopatikana katika ukurasa wa haki miliki wa muhtasari wa somo la Stadi za Kazi. Watahiniwa hao waliweza kuainisha taarifa kama vile; (a) *Alama ya hakimiliki na mwaka wa toleo*, (b) *Namba ya kitabu kimataifa*, (c) *Jina la mwandaaji wa muhtasari huo na anwani yake* na (d) *Tamko la kisheria la kulinda kitabu*. Ufaulu huu ilitokana na uelewa wa kutosha wa mada ya Maandalizi ya Ufundishaji.

2.1.2 Swali la 2: Ushonaji wa Nguo

Swali liliwataka watahiniwa kutaja mambo manne ya msingi ambayo fundi cherehani anapaswa kuyazingatia kabla ya kufanya kazi ya kutarizi nguo. Swali hili lilijibowi na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 1,335 (40.8%) walipata

alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 1: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa, watahiniwa 239 (7.3%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 ambao ni ufaulu mzuri, watahiniwa 1,096 (33.5%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 1,939 (59.2%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 1,335 (40.8%) walipata ufaulu kuanzia wastani kwenda juu katika swali hili. Hii ilitokana na kuwa na uelewa wa kina wa matakwa ya swali na umahiri wa kutosha kuhusu *Ushonaji wa Nguo*. Hivyo waliweza kutaja kwa usahihi mambo ya msingi ambayo fundi cherehani anapaswa kuzingatia kabla ya kufanya kazi ya kutarizi nguo. Miongoni mwa mambo waliyoyataja ni pamoja na; (a) *Nguo unayotaka kutarizi iwe imekwisha katwa au kushonwa*, (b) *Njia utakayotumia kutarizi iwe inafaa kulingana na aina ya kitambaa ulinacho*, (c) *Kama nguo unayotarizi utataka kuifua mara kwa mara ni muhimu uangalie aina ya mishono na nyuzi utakazotumia na* (d) *Kuzingatia kutarizi kwa uzuri na unadhibfu, zisiwepo nyuzi zinazoning'inia upande wa nje au ndani ya nguo*. Hata hivyo, watahiniwa wachache

walitoa hoja mbili au tatu na wengine walitoa hoja ambazo maelezo yake hayakutosheleza, hivyo walipata ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

2	i) Ngoo inapaswa iwe tayari imesha shonwa.
	ii) Kama vazi ni la kufuliwa mara kwa mara azingatia nyuzi na msisho afaka tumia wakati wa kutanzi
	iii) Achague nyuzi za kutanzi kulinga na na aina ya kitambaa na rangi ya kitambaa
	iv) Kuzingatia unadhiifu katika bida rizi kuepukinga kuacha ngoo na nyuzi zinazo ninginia.

Kielelezo Na. 2. 1: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa aliweza kuainisha mambo manne ya msingi ambayo fundi anapaswa kuyazingatia kabla ya kutarizi. Hivyo kupata alama za juu katika swali hili.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,939 (59.2%) waliopata ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya ushonaji na kutarizi. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika vifaa vinavyohitajika katika kushona badala ya mambo ya kuzingatia kabla ya kutarizi kwa kutoa majibu kama vile; *Anatakiwa awe na ujuzi wa kudarizi, Anatakiwa awe na mashine ya kudarizi, Anatakiwa awe na uzi na Anatakiwa awe na mkasi*. Kadhalika, baadhi ya watahiniwa walitoa hoja pungufu na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *Ngoo iwe imeishashonwa, Aina ya mapambo yaendane na ngoo na Utofauti wa ngoo ya kike na ya kiume, mtoto na mkubwa katika kutarizi*.

Vilevile, watahiniwa wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Mfano, mtahiniwa mmoja aliainisha hatua mbalimbali za kushona nguo kwa kutoa majibu kama vile; *Kuchora*

vigezo kwa vipimo sahihi, kukata vigezo, kushona vigezo hatua kwa hatua na kushona nguo kwa kutumia vigezo. Watahiniwa wengine walitoa majibu yaliyohusu aina za mishono ya kutarizi. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *Mwiba wa samaki, Kikonyo na Myororo*. Hii ilipelekea watahiniwa kupata alama za chini na hivyo kuwa na ufaulu hafifu. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

2	<p>i) Kuandaa nipa vya kufanya udanizi kama vile ulizi, sindano na ukasi?</p> <p>ii) Kuweka alama kuonye nguo ungvotaka kudanizi?</p> <p>iii) Kuchoma sindano yenye ure chini ya nguo na kuvutia juu</p> <p>iv) Kuendelea kufundisha alama hadi kukanishe naunguliko wa kudarizi?</p>

Kielelezo Na. 2. 2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa aliainisha hatua za kutarizi badala ya kuainisha mambo manne ya msingi ambayo fundi anapaswa kuyazingatia kabla ya kutarizi. Hivyo kupata alama za chini katika swali hili.

2.1.3 Swali la 3: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha mbinu nne zinazoweza kutumika katika kufundisha ufugaji wa bata kwa wanafunzi wa Darasa la Nne. Jumla ya watahiniwa 3,274 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 3,134 (95.8%) walipata alama kati ya 2.0 hadi 4.0. Jedwali Na. 2 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.

Jedwali Na. 2: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia (%)
0.0 – 1.5	140	4.2
2.0 – 2.5	25	0.8
3.0 – 4.0	3109	95.0

N=3274

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa, watahiniwa 3,109 (95.0%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 ambazo ni ufaulu mzuri, watahiniwa 25 (0.8%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 ambazo ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 140 (4.2%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 ambazo ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 3,134 (95.8%) walipata ufaulu mzuri katika swalii hili kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya *Ufugaji*, hususan ufugaji wa bata. Vilevile, uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa walielewa matakwa ya swalii, hivyo waliweza kubainisha mbinu zinazoweza kutumika katika kufundisha ufugaji wa bata kwa wanafunzi wa Darasa la Nne. Baadhi ya majibu yaliyotolewa ni kama vile; *Majadiliano*, *Kualika mgeni*, *Onesho mbinu*, *Ziara ya kutembelea baadhi ya maeneo ya ufugaji*, *Mbinu ya mhadhara na Kazi mradi*. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walitoa hoja mbili mpaka tatu pekee kati ya hoja nne zilizohitajika na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, hivyo kupelekea watahiniwa hao kupata ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swalii hili kwa usahihi.

3	i) Mbinu ya Ziara -> kuwanawezesha wanafunzi kiongozi na kitembelea sehemu zimzishusisha na ifugaji wa bata
	ii) Onyesho mbinu -> Mamsaidia muunganuzi kushiriki katika batua na vitembo vya utunzaji wa bata
	iii) Mbinu ya majadiliano -> Muunganuzi atawezza kujidili namna zo kuteunzo bata kuna namna sahihi
	iv) Mbinu ya Maswali na majibu -> Mwongezo wa maswali itamwenzesha muunganuzi kujifunzo ifugaji wa bata

Kielelezo Na. 3. 1: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swalii la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa aliweza kubainisha na kuzielezea kwa usahihi mbinu zinazoweza kutumika kufundisha ufugaji wa bata kwa wanafunzi wa Darasa la Nne, hivyo kupata alama za juu katika swali hili.

Aidha, uchambuzi zaidi umeonesha kuwa, watahiniwa 140 (4.30%) waliopata ufaulu hafifu, wengi wao hawakuelewa matakwa ya swali. Hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Baadhi ya watahiniwa walielezea namna ya kufuga bata na wengine walielezea hatua za maandalizi ya ufugaji wa bata. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *Kuchagua eneo la kutengeneza banda*, *Kutengeneza banda*, *Kununua vifaranga bora au mbegu bora ya bata na Kuzingatia kuwapatia chakula na chanjo ya magonjwa mbalimbali*. Mtahiniwa mwingine alitoa majibu kama vile; *Kuchagua aina ya bata unaotaka kufuga*, *Kuandaa banda bora la kufugia bata*, *Kuwapa chakula na chanjo na Kufanya usafi mara kwa mara katika banda*. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuelewa swali hivyo walitoa majibu tofauti na walivyoulizwa. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

3	(i) <i>kuandaa mazingira ya kufugia bata</i> .
	(ii) <i>kuandaa banda la kufugia bata</i>
	(iii) <i>kuandaa chanjo itakayotumika kuchanjia bata</i> .
	(iv) <i>kuandaa chakula cha bata ambacho watakula bata wa kufugusa</i> .


Kielelezo Na. 3. 1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alielezea hatua na maandalizi ya kuanza ufugaji wa bata badala ya kubainisha mbinu zinazoweza kutumika katika kufundisha ufugaji wa bata kwa wanafunzi wa Darasa na Nne, hivyo kupata alama za chini katika swali hili.

2.1.4 Swali la 4: Biashara Ndogo Ndogo

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha vyanzo vinne vinavyoweza kutumiwa na mfanyabiashara mdogo kupata fedha za mtaji. Swali hili

lilijibiwa na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa ni mzuri kwani watahiniwa 3,093 (94.5%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 2: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, watahiniwa 2,989 (91.3%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 amba ni ufaulu mzuri, watahiniwa 140 (3.2%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 amba ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 181 (5.5%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 amba ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 3,093 (94.5%) walipata ufaulu mzuri katika swali hili kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Biashara Ndogo Ndogo*. Watahiniwa hao waliweza kubainisha vyanzo vinne vinavyoweza kutumiwa na mfanyabiashara mdogo kupata fedha za mtaji. Majibu yaliyotolewa ni kama vile; *Kuuza baadhi ya mali alizokuwa nazo mfano mifugo na mashamba, Mikopo kutoka vikundi mbalimbali mfano, UPATU, SACCOSS na VIKOBA, Kutumia akiba aliyokuwa amejiwekea, Zawadi kutoka kwa marafiki, Kuweka akiba na Kuuza kitu chake cha thamani mfano dhahabu*. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa walielewa vizuri matakwa ya swali hivyo kujibu kwa usahihi.

Aidha, watahiniwa wachache waliweza kutoa hoja mbili au tatu kati ya hoja nne zilizohitajika na watahiniwa wengine walichanganya hoja sahihi

na zisizo sahihi, hivyo kupelekea kupata ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

4	
	i) <i>kuuza vitu kama Shamba, mbuzi, kuuza kupata mtaji wa kuanzia biashara,</i>
	ii) <i>kuombaa Msaa da kua ndungu jamaa Na marafiki na hatimaye kuanzisha biashara kwa Sababu umepata mtaji,</i>
	iii) <i>ku chukua mkuopo Mkuopo ni chanzo zia cha kupata mtaji wa kuane a biashara mfano kuchukua Mkuopo benki</i>
	iv) <i>kujinga kuonye vikundi kama Sakso dia hata kujusanya hela na kuweka kuonye sanduku Hatimaye kupata mtaji</i>

Kielelezo Na. 4. 1: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa aliweza kubainisha vyanzo vinne vinavyoweza kutumiwa na mfanyabiashara mdogo kupata fedha za mtaji hivyo, kupata ufaulu mzuri.

Aidha, uchambuzi zaidi umeonesha kuwa, watahiniwa wachache 181 (5.5%) walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Biashara Ndogo Ndogo, hivyo kupelekea kutoa majibu yasiyo sahihi. Mfano mtahiniwa mmoja alitaja mambo yanayoweza kupelekea biashara isifanikiwe kama vile; *Kuwa na mtaji mdogo katika biashara, kutojiweza katika mtaji wake, kutokuwa na ujuzi wa kufanya biashara na kutafuta sehemu isiyo sahihi kwa biashara.* Watahiniwa wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo waliandika aina mbalimbali za biashara badala ya vyanzo vinavyoweza kutumiwa na mfanyabiashara mdogo kupata mtaji. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *Kuzalisha na kuuza, Kununua na kuuza, Kutoa huduma na Machinga au ujasili amali.* Mtahiniwa mwagine alitoa mifano ya biashara ambazo mtu anaweza kufanya kama vile; *Uuzaji wa mbogamboga, Uuzaji wa matunda, Uuzaji wa mandazi na Uuzaji wa pipi.*

Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

4	<p>i) Kutoa huduma mbalimbali katika jami; kama vile kuwa wataala kubeba mizigo</p> <p>ii) kuzalisha bidhaa na kuzaa bidhaa hiyo Mfano kuzalisha nifoga.</p> <p>iii) tununua bidhaa na kuzaa bidhaa Mfano tununua agunira la sukari na kenza kuzaa kidego kidego.</p> <p>iv) kuwa mjasiriamali wa viti Mfano kuteensieneze sabuni, kaki na kupima vitambaa.</p>
---	---

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa alibainisha aina mbalimbali za biashara ambazo mfanyabiashara mdogo anaweza kuzifanya badala ya kubainisha vyanzo vinne vinyloweza kutumiwa na mfanyabiashara mdogo kupata fedha za mtaji hivyo, kukosa alama na kupata ufaulu hafifu.

2.1.5 Swali la 5: Ufundishaji

Swali hili liliwa na vipengele viwili. Kipengele (a) kiliwataka watahiniwa kueleza dhana ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia kama inavyotumika katika somo la Stadi za Kazi na (b) kubainisha faida tatu za kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa ni mzuri kwani watahiniwa 3,256 (99.5%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Jedwali Na. 3 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.

Jedwali Na. 3: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia (%)
0.0 – 1.5	18	0.5
2.0 – 2.5	06	0.2
3.0 – 4.0	3250	99.3

N=3274

Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa, watahiniwa 3,250 (99.3%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 ambazo ni ufaulu mzuri, watahiniwa 06 (0.2%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 ambazo ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 18 (0.5%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 ambazo ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 3,256 (99.5%) walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri katika swali hili. Hii ilisababishwa na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Ufundishaji*, pamoja na kuelewa vizuri matakwa ya swali. Katika kipengele (a) watahiniwa wengi waliweza kuelezea kwa ufupi dhana ya zana za kufundishia na kujifunzia. Majibu yaliyotolewa ni kama vile; *Ni vifaa mbalimbali vinavyotumiwa na mwalimu na mwanafunzi ili kurahisisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji darasani na Zana ni vifaa vyote ambavyo hutumiwa na mwalimu katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji.*

Vilevile, katika kipengele (b), watahiniwa wengi waliweza kubainisha faida tatu za kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi ya majibu yaliyotolewa ni kama vile; *Husaidia mwanafunzi kuwa na kumbukumbu za kudumu, Humsaidia mwalimu kueleweka kwa haraka na kuweza kufikia lengo, Humsaidia mwanafunzi kujenga ari ya udadisi na kulipenda somo, Hurahisisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwani mwalimu hatumii maneno mengi katika ufundishaji na Mwalimu hufundisha kwa kujiamini.* Hata hivyo, watahiniwa wachache waliweza kutoa hoja moja au mbili pekee kati ya hoja tatu zilizohitajika na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi hivyo kupata ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 5.1

kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyweweza kujibu swali hili kwa usahihi.

(a)	Zana za kufundishia na kujifunzi ni vitu vyaote vinywajotumika katika mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji ili Kurahisisha mtaa kato huo na kujifunzo walengwa kuelewa zaidi.
b) i) ii)	Zana huwezo kujenga kumbukumbu nzuri kwenye mwanafani.
ii)	Matumizi ya Zana za kufundishia na kujifunzi huwezo kujifunzo mwanafani kuelewa somo haraka.
iii)	Kutumia Zana Katika Kufundishia na kujifunzi humfanya mwalimu Kufundishia kwa kujifunzi na kujifunzo nafasi kwa somo Lalce.

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa alielezea dhana ya zana za kufundishia na kujifunzia katika kipengele (a) na vilevile alibainisha faida tatu za kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji kwenye kipengele (b), hivyo kupata alama za juu katika swali hili.

Pamoja na ufaulu mzuri katika swali hili, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 18 (0.5%) walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Baadhi yao walainisha mifano halisi ya zana za kufundishia badala ya faida za kutumia zana katika ufundishaji. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu kama vile; *Chati za michoro mfano michoro ya mabwawa ya samaki, mizinga ya nyuki na misitu, Vifaa vya upishi mfano sufuria, sahani, mwiko na kijiko, Ala za muziki mfano zeze, gitaa na baragumu na Vitu halisi mfano mafuta ya mboga.*

Aidha, watahiniwa wengine walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Ufundishaji*, hususani matumizi ya zana katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii ilipelekea kutoa majibu yasiyohusiana na swali. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *Kurahisisha ufanyakaji wa stadi za kazi katika*

usafi na mpangilio maalum mfano matumizi ya jiko, Kutunza mazingira yanayokuzunguka mfano upakaji wa rangi kwa brashi na Kujifunza mahiri mbalimbali muhimu kwa njia ya sauti mfano ngoma. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


o) Stadi za kazi : Ni somo ambalo mtu anapata maarifa stadi' na ujuzi' wa kubuni kutengeneza na kuunda kute. Mfano ujuzi' wa kupitka na ujuzi' wa kufua.
b) i) Huseinidio kuweza kuongeza kipata kwa kufanya kazi mfano kupitka vitafanwa
ii) Husaidia kuweza kuongeza kujingirishwa wenyewe Iswa sababu tunakuwa tumepeata ujuzi' wa kufanya jambu
iii) Husaidia kuweza kuongeza ilivyo wa kuona fursa kutohama na kujifunza somo la stadi za kazi' mfano kufuga kuku, bata, ngombe na somaki.

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa alielezea faida za somo la Stadi za Kazi badala ya faida za kutumia zana katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi hivyo kupata alama za chini katika swali hili.

2.1.6 Swali la 6: Udobi

Swali hili liliwataka watahiniwa kwa kutumia hoja mbili, kuelezea kwa kifupi umuhimu wa kupitisha pasi kwenye kitambaa cha kujaribia kabla ya kuanza kupiga pasi nguo. Swali hili lilijibowi na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa ni mzuri kwani watahiniwa 3,127 (95.5%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 3: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, watahiniwa 2,309 (70.5%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 ambao ni ufaulu mzuri, watahiniwa 818 (25.0%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 147 (4.5%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 3,127 (95.5%) walipata ufaulu wa wastani hadi mzuri katika swali hili. Hii ilitokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Udobu* pamoja na kuelewa vizuri matakwa ya swali. Watahiniwa wengi waliweza kuzielezea sababu za kupitisha pasi kwenye kitambaa kabla ya kuanza kupiga pasi nguo. Baadhi ya majibu yaliyotolewa ni kama vile; *Ili kuweza kubaini ama kujua kiasi cha moto ambaou upo katika pasi ili kuepusha kuunguza nguo, Pia ni kwa sababu ya kuondoa uchafu uliopo chini ya pasi ambaou ungeweza kuchafua nguo.* Majibu mengine yaliyotolewa ni kama vile; *Kujaribu joto la pasi kwa lengo la kuepusha madhara kutokea katika nguo, Kuondoa uchafu uliopo kwenye pasi ili usiweze kuchafua nguo.* Hii inaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha ndio sababu waliweza kutoa majibu kwa usahihi. Hata hivyo, watahiniwa wachache waliweza kutoa hoja moja bila maelezo ya kutosheleza na wengine

walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, hivyo kupelekeea kupata ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

6	<p>① <i>Kuungalia iuapo kiuangap cha moto kinachoa → Kupitisha pasi kwenye kitambaa itatuvaidia kujula iuapo moto ulioveka ni mhalii sans unaowea bupelekaa kuungua nguo.</i></p> <p>② <i>Kuungalia iuapo pasi inachafu unaowea kuchajua nguo. → Kuua usakati pasi hushikq juchafu kua chini mfano ieg uchafu hyo ni kuru, hivyo tunapiti cha ili kuondoa uchafu unaowea kuchafu nguo unayo ipasi.</i></p>

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa aliweza kuelezea kwa ufupi, umuhimu wa kupitisha pasi kwenye kitambaa cha kujaribia kabla ya kuanza kupiga pasi nguo, hivyo alipata alama za juu katika swali hili.

Aidha, uchambuzi zaidi umeonesha kuwa, watahiniwa 147 (4.5%) waliopata ufaulu hafifu, wengi wao walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika umuhimu wa kunyoosha kitambaa kinachotandikwa kwenye meza badala ya kuelezea umuhimu wa kupitisha pasi kwenye kitambaa cha kujaribia kabla ya kuanza kupiga pasi. Mfano, mmoja wa watahiniwa aliandika majibu kama vile; *Kuua wadudu na bakteria waliopo kwenye kitambaa wasioonekana kwa macho ili wasiingie kwenye nguo na Kukinyoosha ili unapoweka nguo yako kisiwe chanzo cha mikunjo isiyohitajika kwenye nguo yako.* Mtahiniwa mwingine aliandika; *Kuondoa mikunjo iliyopo kwenye kitambaa na Kuua vijidudu vilivyomo kwenye shuka au kitambaa.* Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja zilizohusu umuhimu wa kupiga pasi nguo. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *Husaidia kuwa nadhifu wakati wote na hivyo kutuepusha na magonjwa na Husaidia kuua vijidudu vilivyojishikiza kwenye nguo.* Hii

inaonesha kuwa, watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kupelekea kupata alama za chini. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


6	i). Husaidia kuna vijidudu vilinyo ko Kuonye kitambaa hicho; ambaa jo kama usingo nyosha kuanza hata nguo ambayo itauka juu itakuwa inapata vijidudu kutoka kuonye kitambaa a uticho jarabia.
	ii). Ifusaidia kutoa mikunjo ili hato ukuuuka nguo juu isiuze kuna na mikunjo tano batu nayo injooke. Uzuri.

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali hivyo alielezea umuhimu wa kunyoosha kitambaa cha kujaribia badala umuhimu wa kujaribu pasi kabla ya kuanza kupiga pasi nguo, hivyo kupelekea kupata alama za chini katika swali hili.

2.1.7 Swali la 7: Kilimo, Ufugaji na Uvumi

Swali hili liliwataka watahiniwa kuelezea kwa ufupi umuhimu wa kudumisha afya njema ya ng'ombe wa maziwa. Swali lilijibowi na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri kwani jumla ya watahiniwa 2,465 (75.3%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 4: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, watahiniwa 1,795 (54.8%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 ambao ni ufaulu mzuri, watahiniwa 670 (20.5%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 809 (24.7%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 2,465 (75.3%) walipata ufaulu wa kuanzia wastani hadi mzuri katika swali hili. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Kilimo, Ufugaji na Uvuvi*, hususani katika ufugaji wa ng'ombe na uelewa mzuri wa matakwa ya swali. Hii ilipelekea kutoa majibu sahihi kuhusu umuhimu wa kudumisha afya njema ya ng'ombe wa maziwa. Baadhi ya hoja zilizotolewa ni kama vile; *Huwawezesha ng'ombe kuwa na afya bora, Humsaidia ng'ombe asishambuliwe na magonjwa mbalimbali, Humsaidia mfugaji kupata maziwa mengi zaidi, Hupunguza gharama za matibabu, Humsaidia kuepukana na magonjwa, Humsaidia kukua na kunawiri vyema, Husaidia kupunguza gharama zisizokuwa za lazima kwa mfugaji mfano kumtibu ng'ombe na Husaidia kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha maziwa*

nchini. Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa wachache waliweza kutoa hoja mibili au tatu na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo kupata ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliweza kujibu swali hili kwa usahihi.

7	<p>i/ Itacusha magonjira kwa ng'ombe.</p> <p>Hii ina maana yakuwa endapo afya njema itazungatiwa kwa ng'ombe wa mazwa hawatawez kupata magonjira kwa uratini</p>
	<p>ii/ Itasaidia ng'ombe kuwa na afya nzuri Endapo kanuni hii itazungatiwa itawezeku taktu budumisha afya nzuri kwa ng'ombe</p>
	<p>iii/ Itasaidia kuongezeka kuwa kuingo cha maenye yarayopatikaro; Endapo kanuni ya afya njema kwa ng'ombe itazungatiwa mazwa kuongezeka.</p>
	<p>iv/ Itasaidia kuepusha gharano zisizo za lazima; Hii ina mdana yakuwa kanuni ya afya njema itazung atiwa basi usumbufu wa burunuo dawa za mazwakarimaro itauha</p>

Kielelezo Na.7.1: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa aliweza kutoa hoja nne na kuelezea kwa usahihi umuhimu wa kudumisha afya njema ya ng'ombe wa maziwa, hivyo alipata alama za juu katika swali hili.

Kwa upande mwagine, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 809 (24.7%) walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Watahiniwa wengi kati ya hawa walitoa hoja kuhusu namna ya kutunza ng'ombe badala ya umuhimu wa kudumisha afya njema kwa ng'ombe wa maziwa. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile;

- (i) *Kuwapatia eneo zuri na safi makazi yao*
- (ii) *Kuwapatia chakula bora na cha kutosha pamoja na maji*
- (iii) *Kuwapatia chanjo na matibabu pale wanapoonesha dalili mbaya ya afya zao*
- (iv) *Kupata ushauri kuhusu kudumisha afya njema.*

Vilevile, mtahiniwa mwagine aliandika;

- (i) *Kuhakikisha kuwa vyombo vya kuwalishia ng'ombe wa maziwa ni usafi na vinapatikana sehemu husika*
- (ii) *Kuwapatia chakula cha kutosha ambacho kitawezesha ng'ombe hao wa maziwa kuwa na afya njema*
- (iii) *Kuwapatia chanjo ili kuweza kudhibiti magonjwa nyemelezi kwa ng'ombe hao wa maziwa.*

Aidha, majibu mengine yaliyotolewa ni kama vile; *Kwa kuzingatia usafi wa maji na chakula anachopewa ng'ombe wa maziwa, Kuzingatia usafi wa vyombo anavyotumia kulia chakula na kunywea maji ng'ombe wa maziwa, Kuzingatia uthibiti wa magonjwa kwa ng'ombe wa maziwa kwa kumpa chanjo na Kuzingatia usafi wa sehemu anayolala ng'ombe wa maziwa.* Majibu haya yanaonesha kuwa, watahiniwa hakuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi na kupata alama za chini katika swali hili. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


7	<p>i) Ng'ombe wa maziwa wanahitaji lishie bora.</p> <p>ii) Ng'ombe wa maziwa wanahitaji magi safi kuwajiri ya kunywa</p> <p>iii) Ng'ombe wa maziwa wanahitaji bandi lao tenye madarisha makubwa kuwajiri ya kuperisha hewa</p> <p>iv) Ng'ombe wa maziwa wanahitaji chanjo na dawa ya kuwapurizira kyanani kuwapileka soshoto</p>

Kielelezo Na.7.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.2, mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali hivyo alibainisha mahitaji muhimu ya ng'ombe wa maziwa ili wakue vizuri badala ya kuelezea umuhimu wa kudumisha afya ya ng'ombe wa maziwa. Hivyo alipata alama za chini katika swali hili.

2.1.8 Swali la 8: Sanaa za Maonesho

Swali hili liliwataka watahiniwa kuainisha mambo manne ambayo Bwana Ambilikile anatakiwa kuyazingatia wakati wa kughani shairi kwenye maadhimisho ya siku ya wanawake duniani. Swali lilijibiwa na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa hafifu kwani jumla ya watahiniwa 1,250 (38.2%) ndio waliopata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 5: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8

Chati Na. 5 inaonesha kuwa, watahiniwa 2,024 (61.8%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 amba ni ufaulu hafifu, watahiniwa 881 (26.9%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 amba ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 369 (11.3%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 amba ni ufaulu mzuri.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 2,024 (61.8%) waliopata ufaulu wa chini walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Baadhi yao walitoa hoja kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga shairi badala ya mambo ya kuzingatia katika kughani shairi mbele ya kadarnasi. Mfano mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama vile; *Vina na mizani, Beti, Mishororo na Kiitikio au kipokeo*. Mtahiniwa mwengine aliandika; *Aina, Mizani, Beti na Kituo*. Aidha, Mtahiniwa mwengine alichambua vipengele vya fasihi simulizi kutoa hoja kama vile; *Uwepo*

wa jukwaa, Uwepo wa shairi, Uwepo wa hadhira na Uwepo wa fanani. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga na mambo ya kuzingatia wakati wa kughani shairi hivyo kupelekea kupata ufaulu wa chini. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

8	<p>i) Larima aringatie kichwa husika cha Shairi hilo. Mfano. "Maadhimisho ya siku ya Wanawake duniani".</p> <p>ii) Larima aringatie Vina vya Kati na vya Muwisha Viendane katika Shairi hilo.</p> <p>iii) Larima aringatie idadi ya Silabi kati ka kila Metari kwenye Ubeti mang'anya.</p> <p>iv) Larima aringatie kituo kwa kila beti kwa kuhumia Metari ambao Unati via Mkazo wa Shairi hilo.</p>
---	---

Kielelezo Na. 8.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali hivyo alibainisha mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutunga shairi. Hivyo kupata alama za chini katika swali hili.

Kadhalika, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,250 (38.2%) walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Sanaa za maonesho, hususani katika Ushairi. Vilevile, watahiniwa walielewa matakwa ya swali hivyo waliweza kutoa majibu sahihi. Mfano wa hoja zilizotolewa ni kama vile; *Kughani kwa sauti nzuri na ya kuvutia, Azingatie matumizi ya lugha sahihi, Azingatie matumizi ya sauti inayosikika, Utamkaji sahihi wa maneno yaliyopo kwenye shairi hilo ili liweze kueleweka, Kuzingatia ujumbe wa shairi kama ni la huzuni aimbe kihuzuni na kama ni la furaha aimbe kwa furaha*. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.


8	
	i) Kutoa usati inayosikika mbele ya kadamnasi.
	ii) Msimamu muwafaka mbele ya kadamnasi katika kughani shairi hilo.
	iii) Matamshi sahihi ya lugha iliyotumika katika shairi hilo.
	iv) Uzingatiaji wa ujumbe uliopo katika shairi arahalighani.

Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa aliweza kuainisha mambo manne na kutoa hoja sahihi ambazo zilionesha kuwa alielewa swali vizuri. Hivyo alipata alama za juu katika swali hili.

2.1.9 Swali la 9: Muziki

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha mbinu nne watakazowaelekeza washiriki wa mashindano ya kuimba ya *Bongo Star Search* ili waweze kuimba vizuri. Swali lilijibiwa na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa wa wastani kwani jumla ya watahiniwa 2,072 (63.3%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 6: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, watahiniwa 2,072 (43.8%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 ambao ni ufaulu mzuri, watahiniwa 637 (19.5%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 1,202 (36.7%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 2,072 (43.8%) waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya muziki, vilevile walielewa matakwa ya swali, hivyo waliweza kutoa majibu sahihi. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa ni kama vile; *Sauti iendane na mapigo ya muziki, Mpangilio wa sauti kwa kufuata mapigo ya muziki, Wazingatie kupanda na kushuka kwa sauti, Wazingatie mikao wakati wa uimbaji, Kuimba kwa mpangilio wa sauti, Kuimba kwa sauti au kutoa sauti wakati wa kuimba, Kufuata ala za muziki, Kwa kufuata mapigo ya sauti, Utamshi mzuri wa maneno na Kutoa sauti inayosikika vizuri*. Pamoja na hoja hizo, mbinu nyingine wanazoweza kuelekezwa ni kama vile; *Kutawala mpumuo wakati wa kuimba, Jifunze namna ya kurekebisha nota za muziki na kuimba kwa usahihi kufuatana na sauti, Mwili uwe huru na kuyumba kama ni lazima, Uimbaji lazima ufanyike katika sehemu yenye hewa nzuri*. Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

9	<p>i/ Wazingatie kupanda na kushuka kwa sauti ili muimbaji yeote awere kuonekera kuwa anauinba vizuri anatakiwa kuengatio kufanya na kushuka kwa sauti</p> <p>ii/ Utamshi mzuri wa maneno Muimbaji yeote ambayo ni matini kuweza kuimba hukui matamshi ya maneno yanasikika uema kabisa</p> <p>iii/ Kuonekera na mapigo ya muziki Inaweza kuwa makofu, Alimbi, Zere, ngomea nik anatakiwa azingatia mapigo yake.</p> <p>iv/ Mpangilio wa sauti Pia ili muimbaji awere matili anatakiwa kufangilio sauti</p>
---	---

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa aliweza kubainisha kwa usahihi mbinu nne za kuwaelekeza washiriki wa mashindano ya *Bongo Star Search* ili waweze kuimba vizuri. Hivyo kupata alama za juu katika swali hili.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 1,202 (36.7%) waliopata ufaulu hafifu walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Wengi wao walitoa hoja kuhusu mbinu za kufundishia mada hii darasani badala ya kuelezea mbinu za kutumia ili washiriki waweze kuimba vizuri. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile;

- (i) *Majadiliano – Kuwagawa katika makundi na kuadiliana kwa pamoja namna ya kuimba.*
- (ii) *Onesho mbinu – Kwa kuimba ili baadae nao waimbe.*
- (iii) *Igizo dhima – Katika mbinu hii tutaimba kwa kutenda wote kwa pamoja.*
- (iv) *Maswali na majibu – Kwa sababu katika mbinu hii nitamuuliza mshiriki maswali na baada ya kujibu mitajua ni namna gani ninaweza kumsaidia.*

Kadhalika, mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile; *Onesho mbinu, Muhadhara, Mbinu ya ziara na Kumualika mgeni*. Majibu haya yanaonesha jinsi ambavyo watahiniwa hawa hawakuelewa swali hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi na kusababisha kupata alama za chini. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

①	Onesho mbinu, waweze kuona namna yu kuimba vizuri, kupanda na kishuka kwa sauti.
②	Muhadhara, nitawelekera namna yu kuimba vizuri kwa kusigatia sheria kanuni na taratibu za kuimba.
③	Mbinu ya ziara, kuenda sehemu mbalimbali na kuona wati wanawimba mfano katilisa sehemu za studio.
④	Kumualika mgeni, mbinu hii ni ya kumulita mzeupe au wti ambaye anayizuri mikubwa wa kuhusu matuola ya kuimba zaidi yanayu.

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alibainisha mbinu zinazotumika katika kufundisha mada husika badala ya kubainisha mbinu atakazowaelekeza washiriki wa shindano la *Bongo Star Search* ili waimbe vizuri, hivyo kupata alama za chini katika swali hili.

2.1.10 Swali la 10: Sanaa za Maonesho

Swali hili liliwataka watahiniwa kuchambua kwa kifupi faida nne za kutumia onesho mbinu katika kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Nne namna ya kuigiza. Swali lilijibiwa na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri kwani jumla ya watahiniwa 3,264 (99.7%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Jedwali Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.

Jedwali Na. 4: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10*

Alama	Idadi ya Watahiniwa	Asilimia (%)
0.0 – 1.5	10	0.3
2.0 – 2.5	23	0.7
3.0 – 4.0	3241	99.0

N=3274

Jedwali Na. 4 linaonesha kuwa, watahiniwa 3,241 (99.0%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0 ambazo ni ufaulu mzuri, watahiniwa 23 (0.7%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 ambazo ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 10 (0.3) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 1.5 ambazo ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 3,471 (99.7%) waliopata ufaulu wa kuanzia wastani hadi mzuri katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Sanaa za Maonesho*, vilevile walikuwa na uelewa mzuri wa matakwa ya swali. Watahiniwa wengi walichambua faida za kutumia Onesho mbinu katika kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Nne namna ya kuigiza kwa kutoa hoja kama vile; *Huvutia usikivu kwa wanafunzi, Hujenga udadisi na ubunifu kwa wanafunzi, Hujenga ushirikiano baina ya mwalimu na mwanafunzi au*

mwanafunzi na mwanafunzi, Husaidia kutunza kumbukumbu endelevu, Inakuza ari ya kupenda somo, Huleta motisha na kukuza ari ya kujifunza, Huibua fikra, udadisi na vipaji kwa wanafunzi, Wanafunzi wanakuwa wasikivu na wanaburudika na Husaidia kutatua matatizo/changamoto za wanafunzi kwa haraka. Majibu haya yalipelekea watahiniwa hawa kupata alama za juu katika swali hili.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa wachache waliweza kutoa hoja mbili au tatu na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo kupata ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

10	<p>i/ Onyesho mbinu ina wasaidia wanafunzi kuwa na ari ya kupenda kujipumza zaidi. kwa sababu wanafunzi wengi wanapenda kujipumza zaidi kuwa vitendo kuliko nadharia.</p> <p>ii/ Onyesho mbinu inawajengea wanafunzi kumbulcumba ya muda-mrefu; kwa sababu mwanafunzi anaapajifunza kwa kusisha milango yake-yote ya fahamu kuwa ni vigumu sana kusau.</p> <p>iii/ Onyesho mbinu inasmaldia mwalimu wanafunzi walice kulizenda somo lake.</p> <p>iv/ Onyesho mbinu inasaidia kuvuta usikiva kuwa wanafunzi. Ili wawere kuona jambo ambalo li naigilia na kuwaza kupata nafasi ya kauliza maswali.</p>

Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.1, mtahiniwa aliweza kuchambua kwa usahihi faida nne za kutumia onesho mbinu katika kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Nne namna ya kuigiza hivyo kupata alama za juu.

Kwa upande mwingine uchambuzi unaonesha kuwa, kulikuwa na asilimia ndogo (0.3%) ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa hoja zisizo sahihi. Mfano, mtahiniwa mmoja aliainisha hatua za kuandaa onesho badala ya kuchambua kwa kifupi faida nne za kutumia onesho mbinu kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Nne namna ya kuigiza kwa kutoa hoja kama vile;

- (i) *Inasaidia kupanga mada (Igizo) linahusu nini.*
- (ii) *Husaidia kutafuta wahusika na kuwaandaa kikamilifu.*
- (iii) *Husaidia kuwapanga wahusika katika nafasi zao.*

- (iv) *Husaidia kufanya majaribio kabla ya kwenda kufanya vitendo mbele ya hadhira.*

Aidha, mtahiniwa mwingine alitoa hoja zilizohusu kazi za fasihi simulizi kama vile; *Kuburudisha jamii*, *Kuelimisha jamii*, *Kukuza Sanaa katika jamii* na *Kuonya jamii juu ya fikra au tabia mbovu*. Majibu haya yalipelekea watahiniwa kupata ufaulu wa chini katika swali hili. Kadhalika, kulikuwa na watahiniwa wachache ambao hawakujibu swali hili bila kulijibu. Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

10	<p>① <i>Kusaidia katika kufukisha ujumbe kwa tamu huu ka kipata kuumba</i></p> <p>② <i>Husaidia kupata buryadani ya kielesha kuto kana na kichekesha</i></p> <p>③ <i>Kuelimisha tamii juu ya mombacho ambayo haya au kuigiza katika jamii huyo</i></p> <p>④ <i>Ni chanzo cha ajira na kuwe za kutupata kipato kipatia kumudi chode ya kuigiza katika jamii</i></p>
----	--

Kielelezo Na.10.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10.


Katika Kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa alibainisha faida za Sanaa za Maonesho badala ya kuchambua kwa kifupi faida nne za kutumia onesho mbinu katika kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Nne namna ya kuigiza hivyo kupata ufaulu hafifu katika swali hili.

2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha

Sehemu B ilikuwa na maswali manne ya insha kutoka katika mada za taaluma na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali katika sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu, ambapo ufaulu mzuri ulioanzia alama 10.5 hadi 15, ufaulu wa wastani alama 6 hadi 10 na ufaulu hafifu alama 0 hadi 5.5

2.2.1 Swali la 11: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi

Swali hili liliwataka watahiniwa, kwa kutumia hoja sita kuelezea ni kwanini ni muhimu kwa mkulima kutumia mbegu bora katika ustawishaji wa mboga shambani. Swali lilijibowi na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri kwani jumla ya watahiniwa 3,262 (99.6%) walipata alama kuanzia 6.0 hadi 15.0. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 7: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, watahiniwa 2,934 (89.6%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15.0 ambaa ni ufaulu mzuri, watahiniwa 328 (10.0%) walipata alama kuanzia 6.0 hadi 10.0 ambaa ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 12 (0.4%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 5.5 ambaa ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 99.6 ya watahiniwa waliopata ufaulu mzuri na wastani walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Kilimo, Ufugaji na Uvuvi* na vilevile walielewa mahitaji ya swali. Watahiniwa hawa waliweza kuelezea kwa usahihi umuhimu wa mkulima kutumia mbegu bora katika ustawishaji wa mboga shambani. Mfano wa hoja zilizotolewa ni kama vile; *Mbegu bora haziwezi kushambuliwa na wadudu waharibifu, Husaidia kuzalisha mboga nyngi*

kwa muda mfupi, Mbegu bora huzalisha mboga zinazokua haraka, Husaidia kupata mboga bora zinazostawi vizuri, Ili uweze kufanya uzalishaji wenyе tija na kupata maendeleo na Humsaidia mkulima kuinua kipato chake. Aidha, watahiniwa wengine waliweza kutoa hoja sahihi lakini maelezo yao hayakujitosheleza hivyo kuwa na ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyweweza kujibu swali hili kwa usahihi.

11	<p>Ustawiishaji wa mboga hi; ni shughuli ya kili mo cha Bustani ambayo huweza kustawishia mboga ta aina mbalimbali mfano: mbichesi, Bamici, Chaini si, Sukuma wiki na mboga zingine</p> <p>Umuhimu kua mkulima kutumia mbegu bora katika Ustawiishaji wa mboga Shambani ni kama ifuatavye kupata au kuvuna mboga kua wingi au marao mengi; Mkulima anapatumia mbegu bora, huweza ku pata marao mengi anawesta kupata mboga nyingi. Kutokana na mbegu bora alizotumia katika ustawi shaji wa mboga.</p> <p>Kuepuka ubaribifu wa mboga Shambani; kuna wadudu wengi wanawera kusahambulia mboga zinapoku wa Shambani, hiyo mkulima anapatumia mbegubora inawesta, kusaidia kupungura mboga kusahambulia wa kupunguta gharame; mkulima anawero kuu mia gharame katika Ustawiishaji wa mboga Shambani, lakin akitumia mbegu bora zinawesta zikustahimili magonjua na hiyo kupungura gharamezakununua alau ta kudibu mboga.</p> <p>Kupata marao bora; mkulima anapatumia mbegu bora katika Ustawiishaji wa mboga anawero, akapata marao bora mfano, mboga zilizokomaa vizuri, mboga tenye afya lakin ukitumia mbegu mbaya una weza ukapata marao hafifu.</p> <p>Kupata marao kua muda mwafaka; mkuli ma anapatumia mbegu bora anawero kuvuna kua muda maarumu na akavupe marao mengi mbegu mbora n; mahimu sana katika Ustawiishaji wa mboga Shambani.</p> <p>Kuepuka ubaribifu wa rutuba Shambani; mbegu bora huweza kustawis; kua karibu bilo kuharibiu rutuba kua kua hahitaji kutumia madarasi mengi yanayo weza kusababisha rutuba kupata.</p> <p>Hiyo basi; mkulima analakiwa kutumia mbegu bora katika Ustawiishaji wa mboga Shambani; kua kua kua aina mbalimbali ta mboga na zinapende sana mfano mboga ta majani, mboga ta mitili, mboga ta madundu na mboga ta malla.</p>
11 Cont.	

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.1, mtahiniwa alimudu kuelezea umuhimu kwa mkulima kutumia mbegu bora katika ustawishaji wa mboga shambani ingawa katika baadhi ya hoja maelezo hayakujitosheleza sana. Hivyo, alishindwa kupata alama zote 15 katika swali hili.

Aidha, kwa upande mwengine, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 12 (0.4%) waliokuwa na ufaulu hafifu, walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi, hususani kilimo cha mboga mboga. Hivyo walitoa hoja moja au mbili pekee kati ya sita zilizohitajika kwenye swali bila maelezo. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *Mazao yaweze kustawi vizuri, Ili kuongeza mazao*. Vilevile, baadhi ya watahiniwa walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo, kutoa hoja zisizo sahihi. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zilizohusiana na maandalizi na upandaji wa mboga badala ya kuelezea umuhimu wa kutumia mbegu bora katika ustawishaji wa mboga shambani. Aidha, baadhi ya watahiniwa hawakujibu swali hili. Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


11	<p>Mboga ni majani ambayo kuhuniwa na bindeedanu. Kama za chakula ku mfanu mbachi kaa Sipinanchi, na Sulkuma ujiki. Iwara matano mbali mbali za mbogarazo ni mbogazia majani, mbogazia medundu, mbogazia mizzi mbogara mashini na mboga ze manu. Zifuratu zo ni hatua ze kustawistha mbogastha mbani ni kama vite.</p> <p>Kuchaguru mbegu bora, mkulima kabila ya kustawistha mboga Shumba Inampasa kuchaguru mbeu na iyo bora na itakayo stevi.</p> <p>Chagua eneo linalo faa kuhuniwa mboga, mkulima ane Shauliwa kuchaguru eneo amballi kusefaa kwacajili ya kustawistha mboga Shumbani.</p> <p>Tima eneo hilo na kuli sawarisha, mku uruu wa mboga anashauliwa kuhuni Shumba kelle vizuri na kuli sawarisha kwacajiliya kustawisha mboga.</p> <p>Kuweka mbolea na kuchaguru nyasi na udongo mkulima wa mboga anashauliwa ci kuweka mbolea nukucha negara na udongo akali kisti vincachanga nyikina vizuri kuna wa tayari kuweka mbegu.</p> <p>Waka mbegu kwa mistari makutuwajili na kufunika nyasi ikuwa upotevu wa maji. Mkulima anashauliwa bawala kipanda, kwa gitu chakikishi aragunika kwa nyasi ili kuweza kusaidia kuzuka upotevuu wa maji kwa jua ya mvule waka jua krapo (kuweka) nowaka.</p> <p>Baadaya kuota ondo maji na endelea kumwa gitu maji mpaka ukue, mkulima anashauli wa kuendelea kumuwajili maji mpaka mbo zifike wa keri hi na kuhuniwa binadilani.</p> <p>Aiyo basi mkulima anashauliwa kipanda mbogi kwa kungaili kipuli iwa rawa kuna wadudu masi meze kuhalibii kuna mboga ni mbini kwa afya ya binadilani kumanu humpu tafu vitamini miwilini.</p>
11 Cont.	

Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2, mtahiniwa aliaainisha hatua za kuandaa shamba na kupanda mbegu shambani badala ya kuelezea umuhimu wa mkulima kutumia mbegu bora katika ustawishaji wa mboga shambani. Hii ilisababisha mtahiniwa kupata alama za chini katika swali hili.

2.2.2 Swali la 12: Upishi

Swali hili liliwataka watahiniwa kuelezea hatua sita watakazozitumia kuwaelimisha wanafunzi wa Darasa la Tano kuhusu *Upishi wa Ugali*. Swali lilijibiwa na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri kwani jumla ya watahiniwa 3,013 (92.0%) walipata alama kuanzia 6.0 hadi 15.0. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 8: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, watahiniwa 1,717 (52.4%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15.0 ambao ni ufaulu mzuri, watahiniwa 1,296 (39.6%) walipata alama kuanzia 6.0 hadi 10.0 ambao ni ufaulu wa wastani na

watahiniwa 261 (8.0 %) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 3,013 (92.0%) ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri na wastani, wengi wao walijibu swalii hili vizuri kutokana na kuwa na uzoefu wa kutosha wa kupika ugali. Mada ya *Upishi* ni moja ya mada zinazohusisha vitu vinyavyofanyika katika maisha ya kila siku. Hivyo, watahiniwa waliweza kujibu kulingana na uzoefu wa kila mmoja. Aidha, majibu mengi yanaonesha kuwa kuna hatua mbalimbali za kupika ugali. Baadhi ya watahiniwa walichanganya hatua mbili au zaidi kwa pamoja na wengine walianza kwa kutaja maandalizi ya viambaupishi pamoja na jiko. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama vile; *Kubandika sufuria ya maji jikoni, Kuweka unga kiasi na kuendelea kukoroga mpaka uchemke, Kuacha uji uchemke kwa muda kidogo, Kuweka unga kidogo kidogo huku ukiendelea kukoroga au kusonga na Kupakuliwa tayari kwa kuliwa*. Mtahiniwa mwingine aliandika; *Kutia maji katika sufuria na kuyachemsha, Mpishi anatakiwa kukoroga uji, Hatua inayofuata mpishi anatakiwa kusonga ugali kwa kuongeza unga kwenye uji uliochemka vizuri, Mpishi aepue ugali kwa ajili ya kuliwa*. Majibu hayo yalikuwa sahihi hivyo kupelekea watahiniwa kupata alama za juu katika swalii hili.

Aidha, baadhi ya watahiniwa wachache waliweza kutoa hoja tatu mpaka nne pekee kati ya sita zilizohitajika hivyo kuwa na ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swalii hili kwa usahihi.

	<p>Upishi ni hitsendo cha kuandha, kuhayatisha, kuperika na kuperaka chakula tayari kwa haliwa. Zipo hafua nta kazowaelimisha wanafunzi katika somo la upishi wa ugali ambayo ni hizi zifundato; -</p> <p>Antao viambauupishi na vifaa; Pa hii ni hafua ya kuandha katika upishi wa ugali ambayo ni kuandha viambauupishi ambayo ni uga na vifaa ambayo ni sufuria, mafuto ambayo vifatumika katika upishi wa ugali, hahikista vifaa hiyo ni visafi. Hiyo bari hafua ya kuandha katika upishi wa ugali ni kuandha viambauupishi na vifaa.</p> <p>Kuweha maji jikoni ili yapate vuguvugu; Pa bli ni hafua ya pili ya katika upishi wa ugali ambayo ni kuweha maji jikoni ili yapate vuguvugu ili unga usipate mabunge (mabunge bonge) hahikista maji kuyachemka fukuto. Hiyo bari hii ni hafua ya pili ya kuzingatia katika upishi wa ugali.</p> <p>Kuweha unga kiasi na kuanza kutozoga uji mpaka uchemka; Pa hii ni hafua ya tatu katika upishi wa ugali ambayo ni kuweha unga kiasi kotofa maji na kuanza kutozoga mpaka uchemka, kutozoga uji kwa sababu unga usiende kujan chini ya sufuria na kusababisha mabunge mabunge, uji unatakiwa uchemka visuri ili ugali usiwe mbichi. Hiyo bari hii ni hafua ya tatu katika upishi wa ugali.</p> <p>Uji ukichemka visuri westa unga kidogo kidogo huku unasonga mpaka civet; Pa hii ni hafua ya nne katika upishi wa ugali ambayo ni uji ukichemka visuri westa unga kidogo kidogo mpaka civet funawasha unga uji utishachemka visuri ili kusuri ugali usiwe mbichi pa kuweha ugali usiwe na mabunge mabunge, inapagua uweka unga kidogo kidogo huku unasonga ugali mpaka civet.</p>
--	---

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya sehemu ya jibu lililo sahihi katika swali la 12.

Katika Kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa alimudu kuelezea hatua mbalimbali atakazowaelimisha wanafunzi wa Darasa la Tano kuhusu upishi wa ugali

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 261 (0.8%) waliopata ufaulu hafifu, walishindwa kuelewa matakwa ya swalii hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Baadhi ya watahiniwa waliainisha mbinu mbalimbali za kufundishia badala ya kuelezea hatua mbalimbali watakazowaelimisha wanafunzi wa Darasa la Tano kuhusu upishi wa ugali. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama vile; *Kwa kutumia mbinu ya mhadhara*, *Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu*, *Kwa kutumia mbinu ya majadiliano*, *Kwa kutumia mbinu ya maelezo na Kwa kutumia mbinu ya onesho mbinu*. Aidha, mtahiniwa mwingine aliainisha njia mbalimbali za kupika kama vile; *Kukaanga*, *Kuchemsha*, *Kubanika*, *Kuoka na Mvuke*. Kadhalika, watahiniwa wengine walibainisha kanuni za usafi katika mapishi. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *Eneo liwe safi*, *Mpishi awe safi*, *Mavazi yawe safi*, *Chakula kiwe safi*, *Chakula kifunikwe na Vifaa viwe visafi*. Majibu haya yanaonesha kuwa, watahiniwa walishindwa kuelewa matakwa ya swalii hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swalii hili kwa usahihi.


	<p>Hatua ni zefaratibu ambao hufuata Mteririkò ili kuweza kufiki a Lengo lilelo weza Kutarajwa ili kuweza kufanikisha tendozima la upifunzaji na ufundishaji Zifudao ni Hatua ndakazowaelimisha wana Funzi katika somo la Upishi wa Ugali Utangulizi; Hii ni batua yakwanza ombayo nitawaelimisha kwa kunaambia Ugali ni chakula cha Protini ambacho huje ngamwili na Upi kwayi wake nitahutisana Kujenga UMahiri; batua hii nitaa waelekzo kuwa Upishi wa Ugali uhitaji Maandalizi ya Unga, Maji, Sufura, Muiko jiko hivi ndiyo vitu ambayo hutanya ukali Kukamidika kwa kuwasha jiko Kubandika maji, Kukologea, kuchemka na kuanza kusong a Ugali kwa kuweka Unga Ugali kukaaza Kuimarijha UMahiri; nitawaelokaa kwa kutumia zana namna au jinsi ya Upishi wa Ugali kwa Vitendo kwa kuwaonyesha asinga yonye Iqizo La Upishi wa Ugali kuani a Mwanzo hadi kwiisho, kiuachorea picha yonye vifaa vya Upishi wa Ugali au kufanya kwa Vitendo kama kazi mudi darasani Hitimisho; nitawezu kutafuta kufambua Wahafunzi wangu Wamelewa kwa Kuwasanya Upmaji kufotana na kile ambacho nimeueza Kuwaefimasha kwa Kuwapa kashati ya Upishi wa Ugali au Mazoezi kwenye kitabu kujibu kwa kuta bainisha wameuseza kupata Maanifi</p>
--	--

Kielelezo Na. 12.2; Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 12.

Katika Kielelezo Na. 12.2, mtahiniwa alielezea hatua za ufundishaji ambazo zinapatikana kwenye Andalio la Somo badala ya kuelezea hatua mbalimbali atakazowaelimisha wanafunzi wa Darasa la Tano kuhusu upishi wa ugali. Hivyo kupata ufaulu hafifu katika swali hili.

2.2.3 Swali la 13: Ufundishaji

Swali hili liliwataka watahiniwa kufafanua faida sita anazozipata mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anapotumia Andalio la Somo wakati wa ufundishaji. Swali lilijibiwa na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri kwani jumla ya watahiniwa 3,254 (99.6%) walipata alama kuanzia 6.0 hadi 15.0. Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 9: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13

Chati Na. 9 inaonesha kuwa, watahiniwa 1,426 (43.6%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15.0 ambao ni ufaulu mzuri, watahiniwa 1,828 (55.8%) alama kuanzia 6.0 hadi 10.0 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 20 (0.6 %) alama kuanzia 0.0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 99.6 ya watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha na walielewa matakwa ya swali, vievile walikuwa na uwezo wa kujenga hoja hivyo, waliweza kujibu kwa ufasaha. Miongoni mwa majibu yaliyotolewa ni kama vile; *Kufundisha kwa kufuata muda uliopangwa, Mwalimu kufundisha kwa kujiamini, Humsaidia mwalimu kutotoka nje ya mada, Humsaidia mwalimu kufikia malengo mahsususi, Huboresha ufundishaji, Humsaidia mwalimu kutambua mbinu na njia sahihi za ufundishaji wake, Humsaidia mwalimu katika*

kuboresha ufundishaji wake, Humsaidia mwalimu kufanya tathmini ya wanafunzi wameelewa kwa kiasi gani na Humsaidia mwalimu kujua namna ya kutumia zana. Majibu sahihi yalitokana na uzoefu waliopata watahiniwa katika kufanya mazoezi ya kuandaa somo wakati wa kipindi cha mazoezi ya muda mrefu. (Block Teaching Practice). Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

13	<p><i>Andalio la Somo - Huu ni mpango kazi-wa muda mfupi unaandaliwa na Muslimu wa Somo huu ilidwa laipindi kiniwa au viwili idha siku. Ni kweni idha andalio la Somo ni Muslimu Sana tawala muslimu yeyote ytu le arapfundisha. Natiibitisha uliwele huu tawala hoja zifukute Humfanya mwalimu afundisha tawala kujiamini hii ni tawala Sababu atakidhwa na fikra nyingi za tawasitiha kwa wanafunzi tawala Sababu atakumu - ame kifanyia Maendalizie mapema klabla ya kwenetaka tukodi wasilisha tawala wanafunzi darejani nifano atakidhwa na zana za tatuksa mpangilia mzuri wa kazi na - Viti vigeze vigezi ambayo vitamfanya ajiamini.</i></p> <p><i>Humfanya Muslimu afundisha kujua Mtinikiko au mpangilia mzuri, hii ni idha Sababu atakidhwa ame pangilia Maendalizie kikamilifu na kusogea viziui hatua atakazo zifukute ukweli na kufundisha tawala nifano. Ikuuza na utangulizi, kujengwa umuhimmo na - kujiamisha umuhili batiba Somo. <i>hiz</i> idhuyu itensatia.</i></p> <p><i>Humsaidia Muslimu kujanya tathminini baada ya kipindi kwiisha, - Hii ni tawala Sababu pale - anapofundisha tawala weengine labda hawata elewa kutokek na hali au matatizo mbalimbali na kimea tajua ni - Wengapi Wamelewa na ambao hawaje elewa na kumua idubaini utaratibou wa tawasaadia ule ambao wame - Shindua tawalewa batiba sona hili.</i></p> <p><i>Humsaidia batiba kujubanesho mbinyu - za refundishaji hii ni kwe Sababu mwalimu anawa za kujunua mbinyu mbalimbali pale anapofundisha hiz <i>basi aktiona mbinyu ambazo zimekuuza kazi - batihili vigezo anauzeza kujubanishaa ili kujueza kujenda Sambamba na matatizo ytu wanafunzi - bkhulunganana na ulewa wao.</i></i></p>
----	--

13 Cont.	<p>Humsaidia katika kwenda zana au vifaa -</p> <p>Via kufundishaji - hii ni kwa sababu catakwa tayari ameshamali za kwenda Somo na kwenda Kubaini vifaa - au zana zinszo hitajika katika Janguli hiyo mfano - labda Meda ya upishi - mwalimu ataaendaa vifaa vinavyo - huijaa na upishi iti kwenda kueleweka kwenda nafisi .</p> <p>Mwalimu litamsaidia katika Matumizi - Meawu ya muda, hii ni kwa sababu hili kipengelo - bina muda walice kwa hiyo ata kwa anaingi hatua hii - nitumie muda kiasi gani na hili kipengelo binawitoga - gani kulinganisha na muda ambao unatakingi mfano - labda u tangulizi daki 10, lajengi umalimi daki 10 - na kwendelea . hiyo ndinzo itamsaidia Somo .</p> <p>Hivyo basi tunesha umuhimu wa andalio la Somo lakini pia tunapaswa kufahamu madharifu ya kuto tumia andalio la Somo kama vile - kipoteza ha - Maandhi, kipoteza muda, kuto jamiini na madharifu mengine mengi" lakini pia na zenda kutoa ushauri kwa wazimmo wote ni nyumba kwenda andalio la Somo kuwani lina umuhimu m kubwa sang katika tena Zime la ufundishaji na ujifunzaji .</p>
----------	--

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya sehemu ya jibu lililo sahihi katika swali la 13.


Katika Kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa aliweza kufafanua kwa usahihi faida sita anazozipata mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anapotumia Andalio la Somo hivyo aliweza kupata alama za juu katika swali hili.

Pamoja na ufaulu wa juu katika swali hili, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa kulikuwa na watahiniwa 20 (0.6%) waliopata ufaulu hafifu. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zilizohusu matumizi ya zana katika ufundishaji na ujifunzaji badala ya faida sita anazozipata mwalimu wa somo la Stadi za Kazi anapotumia Andalio la Somo wakati wa ufundishaji kwa kuandika; *Humsaidia mwalimu kueleweka kwa haraka, Humsaidia mwalimu kutumia maneno machache, Mwalimu hueleweka vizuri, Mwalimu hushirikiana na wanafunzi, Mwalimu*

kuhusianisha mazingira na mahiri anayofundisha na Mwalimu ataanza na mada rahisi kabla ya ngumu. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile; Humsaidia mwalimu kuvuta usikivu wa wanafunzi, Humsaidia mwalimu kukuza hali ya wanafunzi kupenda somo lake, Humsaidia mwalimu kueleweka kwa haraka. Hata hivyo mtahiniwa alishindwa kuelewa kuwa hoja alizotoa zilihusu faida za kufundisha kwa kutumia zana hivyo kushindwa kupata alama katika swali hili. Aidha, baadhi ya watahiniwa hawakujibu swali hili. Majibu haya yanaonesha kuwa, watahiniwa hawakuelewa swali hivyo kupelekea kupata ufaulu wa chini katika swali hili.

2.2.4 Swali la 14: Upimaji

Swali hili liliwataka watahiniwa kufafanua kanuni sita ambazo mwalimu anapaswa kuzizingatia katika kuandaa maswali ya kuchagua jibu sahihi. Swali lilijibowi na watahiniwa 3,274 (100%). Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani jumla ya watahiniwa 2,599 (79.4%) walipata alama kuanzia 6.0 hadi 15.07 kama ilivyooneshwa kwenye Chati Na. 10.



Chati Na. 10: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14

Chati Na. 10 inaonesha kuwa, watahiniwa 767 (23.4%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15.0 ambao ni ufaulu mzuri, watahiniwa 1,832 (56.0%) alama kuanzia 6.0 hadi 10.0 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 675 (20.6 %) alama kuanzia 0.0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 2,599 (79.4%) walipata ufaulu mzuri na wa wastani. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na umahiri wa kutosha katika mada ya *Upimaji* na vilevile walielewa matakwa ya swali, hivyo waliweza kutoa majibu sahihi. Baadhi ya hoja zilizofafanuliwa ni kama vile; *Maswali yawe na misamiati inayoeleweka, Kuzingatia kuweka majibu yanayoshabihiana, Maswali yasiwe na jibu zaidi ya moja, Hakikisha nafasi ya jibu sahihi inabadilika, Kuepuka kutunga swali kwa kunakili sentensi kutoka kwenye kitabu, Majibu yasiwe na vidokezo vinavyotoa mwanya wa jibu sahihi, Kuepuka kutumia sentensi hasi katika swali, Kuhakikisha kuwa urefu wa sentensi katika majibu hautofautiani sana na Vipotoshi visitofautiane sana na jibu sahihi*. Majibu haya yanaonesha kuwa, watahiniwa walielewa swali vizuri hivyo kupata ufaulu wa juu kwenye swali hili. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa waliweza kutoa hoja tatu mpaka nne pekee badala ya sita zilizohitajika kwenye swali, na wengine walitoa hoja bila maelezo ya kutosheleza, hivyo walipata ufaulu wa wastani. Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

Maswali ya kuchagua jibu salubi ni Maswali yanayonataea unwanafunzi achague vichachawizi tawa tenandi-ka jibu sa au herufi ya jibu salubi kafika swali hilo. Ni, kweli tawa zipo kach tenuri mbali ambali za tari-ngati kafika tenandaa maswali haya kama i fuatanya.

Majibu ya vichachawizi yalingo ne kafika kila swali, Mfano swali la kuanza likiwa na vichachawizi A, B, C, D, na E hiyo hiyo kafika swali la pili vichachawizi vilingane.

Majibu yawe yanabadiilita - badiilita kafika kila swali, Mfano kama swali la kuanza jibu ni A basi jibu la swali la tatu au pili liwe tinabadilita tawa D au chingo tawa fanya wanafunzi tawa wataalar nne kafika kuchagua.

Maswali yasiwe Marefu au sentensi za Maswali zisiwe ndefu tenachosha unwanafunzi, Mfano kafika Maswali yatakayotungwa yasiwe marefu ili tueputka tenachosha unwanafunzi

Kueputka kuitumia kinyume katika kuuliza Maswali, Mfano swali litakalotungwa lisio kinyume kafika kuuliza aina ya swali mfanu kwalikuu J-k-nyerere kahawa rahizi wa

14 Cont.	<p>Tanzama mwaka laici na kuweza magari ambayo yatawafanya wanafunzi wasilie lewe swali katika ufmudishaji na ujifunzaji. Swali hii katika namna ambayo inalewetka kwa urahisi, Mfano swali lietewetka kwa wanafunzi ili kuwayengesha ufitirishaji na uhadisi katika tuchagua vichachawizi.</p> <p>Kuepukta Kutubia Misaniati Miguuuu katika kutunga swali, Mfano swali mu asitania Misaniati Miguuuu ambayo haiteweki tava wanafunzi swali hii katika hali ya uwazi ili mwanafunzi alielewe.</p> <p>Kuepukta kuchukua sentensi za Moja kwa moja kutosha Kitabuni, Mfano swali litakalotungya lisichukuliwe au kumutum kutosha Kitabuni Moja kwa moja.</p> <p>Hivyo basi ni Muhimmo kwa Mwalimu kuzingatia kanuni zilizoelezewa hapo juu ili kuweza kuandaa Maswali bora ya kuchagua jibu sahibi pia Maswali haya yana fida kama vite, ni rahisi kutsalihisha na kutoa alama bila upendo leo.</p>
----------	---

Kielelezo Na. 14.1: Sampuli ya sehemu ya jibu lililo sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa aliweza kufafanua kwa usahihi kanuni sita ambazo mwalimu anapaswa kuzizingatia katika kuandaa maswali ya kuchagua jibu sahihi. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya upimaji hivyo kupata alama za juu katika swali hili.

Kadhalika, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 675 (20.6%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo kupelekea kutoa hoja zisizo sahihi.

Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandaa Jedwali la Utahini badala ya kufafanua kanuni sita anazopaswa kuzingatia katika kuandaa maswali ya kuchagua jibu sahihi. Majibu yaliyotolewa ni kama vile; *Uwepo wa idadi ya mada zilizofundishwa, Uwepo wa idadi ya maswali yanayohitajika, Uwepo wa mada zinazotakiwa kupimwa, Idadi ya maswali katika kila mada na Uzito wa kila mada inayopimwa*. Aidha, baadhi yao walitoa hoja zisizohusiana na swali liloulizwa. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *Kuzingatia uhusiano uliopo kati ya maswali ya kuchagua na jibu sahihi na mada yenye, Madhumuni ya kutunga maswali haya ya kuchagua jibu sahihi, Kuzingatia umri wa walengwa na Kuzingatia kufuatwa kwa mtaala wa elimu kulingana na somo.*

Aidha, watahiniwa wengine walibainisha mambo ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa muongozo wa usahihishaji. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *Kuzingatia mada husika, Kuzingatia uwezo wa wanafunzi, Kuzingatia ugumu wa swali, Kuzingatia kupimwa kwa swali na Kuzingatia utoaji wa alama*. Watahiniwa wengine hawakujibu swali hili. Hii inaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa hawakufanya maandalizi ya kutosha kabla ya kuingia kwenye mtihani. Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

14	<p>Maswali ya kuchagua jibu sahihi; ni ma swali ambayo humfikilisha mwanafunzi; Katika suala zima la ufundishaji na yijifunzaji wa somo husika.</p> <p>Zifuratazo ni Kanuni zinazopaswa kuzingatiwa katika kuaandaa mawali ya kuchagua jibu sahihi kwa walimu zote katika somo husika. Umri wa walengwa; Mwalimu anapochagu liwa kubandaa maswali ya kuchagua jibu sahihi lazima angalie umri wa walengwa wake kwa muda huo huwezi kutunga maswali yanayowazidi umri wanafunzi wako.</p> <p>Uelewa wa wanafunzi; Mwalimu anapo andaa maswali ya kuchagua lazima angali e Uelewa wa wanafunzi wake ukoje ndo gandae maswali kulingana na uelewa wa wanafunzi wake kutokana na swali ya kuchagua jibu sahihi hii itaboresha utungaji.</p> <p>Idadi ya walengwa, Mwalimu anapotunganya maswali lazima angalie darasa lake linawatoto wangapi na kuweza kuandaa ma swali kulingana na Idadi hiyo Kanuni hizi huboresha utungaji wa maswali kwa wanafunzi huparwa kuangalia darasa langu linawinganafunzi wangapi na kuandaa kulingana na idadi.</p> <p>Uhitaji wa wanafunzi; Mwalimu anapo andaa maswali ya kuchagua jibu sahihi lazima e angalie Uhitaji wa wanafunzi wake wanahitaji nini nini na wamejifunza kitu gani hapo utawezo kuendana na wanafunzi kutokana na kujua mabitaji yao kwa muda huo.</p>
----	---

Kielelezo Na. 14.2: Sampuli ya sehemu ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.2, mtahiniwa aliandika baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatia mwalimu anapochagua njia za kufundishia badala ya kufafanua kanuni sita anazopaswa kuzingatia katika kuandaa maswali ya kuchagua jibu sahihi.

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA

Jumla ya mada 10 zilitahiniwa katika mtihani wa somo la Stadi za Kazi. Kati ya hizo, mada sita (6) zilikuwa na ufaulu mzuri kama ifuatavyo: *Ufundishaji* (99.45%), *Udobi* (95.50%), *Biasara Ndogo Ndogo* (94.50%), *Upishi* (92.00%), *Kilimo*, *Ufugaji na Uvuvi* (90.23%) na *Upimaji* (79.40%), Aidha, mada za *Sanaa za Maonesho*, *Muziki na Ushonaji wa Nguo* zilikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 68.95, 63.30 na 40.80 mtawalia. Hata hivyo mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji* ilionekana kuwa na ufaulu hafifu kwa asilimia 15.90. Muhtasari wa ufaulu katika mada umeoneshwa katika Kiambatisho cha Pekee.

Uchambuzi zaidi uliofanyika ulibaini kuwa, ufaulu mzuri katika mada hizo umetokana na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha, uwezo mzuri wa kujenga hoja pamoja na kuelewa matakwa ya swali. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walishindwa kupata alama za juu hususani katika mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji*, hii ilisababishwa na watahiniwa hawa kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana iliyoulizwa, kushindwa kujenga hoja hasa katika kujibu maswali ya insha na kushindwa kuelewa matakwa ya swali.

4.0 HITIMISHO

Matokeo ya uchambuzi wa takwimu za ufaulu kwa watahiniwa yanathibitisha kuwa, kwa ujumla, ufaulu kwa watahiniwa katika somo la Stadi za Kazi ulikuwa mzuri. Maswali ambayo watahiniwa wengi walipata alama za juu yalikuwa kumi (10), wastani maswali mawili (02) na hafifu maswali mawili (02). Aidha, majibu ya watahiniwa yaliyonukuliwa au kuambatishwa kama vielelezo vya majibu mazuri yameonesha kuwa umahiri wa watahiniwa katika dhana zilizoulizwa ulikuwa mzuri. Kwa upande mwingine, mada moja (01) tu ndio iliyokuwa na ufaulu hafifu, jambo linaloonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na umahiri wa kutosha katika mada za somo husika.

5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuongeza kiwango cha ufaulu katika mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji* iliyokuwa na ufaulu hafifu na mada zenyé ufaulu wa wastani yafuatayo yanashauriwa.

- (i) Wakufunzi watumie mbinu mbalimbali za kufundishia kama vile: Bungua bongo. Maswali ambayo yataulizwa yataibua ufahamu walionao wanafunzi na kumuongezea maarifa mapya. Mbinu hizi zitawafanya wanafunzi wapate uelewa mzuri wa mada inayofundishwa.
- (ii) Wakufunzi watumie zana halisi za kufundishia, mfano muhtasari, ili kuona muundo wake na taarifa nne muhimu katika ukurasa wa haki miliki. Hii itaongeza uelewa wa mada husika.
- (iii) Walimu tarajali wasome rejea mbalimbali ili kuiongezea maarifa katika mada ya Maandalizi ya Ufundishaji na somo la Stadi za Kazi kwa ujumla.
- (iv) Watahiniwa waelekezwe kusoma maswali kwa makini na kuyaelewa kabla ya kujibu ili kupunguza changamoto ya kujibu nje ya matakwa ya swalí. Jambo hili linaweza kufanyika kwa walimu tarajali kupewa majaribio, kazi mradi na kazi za nyumbani ilihali wakufunzi watasahihisha na kutoa mrejesho kwa wakati.

Kiambatisho

Na.	Mada	Namba ya swalii	Asilimia ya Ufaulu		Maoni
			Waliopata alama 40 na zaidi	Wastani	
1.	Ufundishaji	5	99.5	99.45	Vizuri
		13	99.4		
2.	Udobi	6	95.5	95.50	Vizuri
3.	Biashara Ndogo Ndogo	4	94.5	94.50	Vizuri
4.	Upishi	12	92.0	92.00	Vizuri
5.	Kilimo, Ufugaji na Uvuvii	11	99.6	90.23	Vizuri
		3	95.8		
		7	75.3		
6.	Upimaji na Tathmini	14	79.4	79.40	Vizuri
7.	Sanaa za Maonesho	10	99.7	68.95	Wsatani
		8	38.2		
8.	Muziki	9	63.3	63.30	Wastani
9.	Ushonaji wa Nguo	2	40.8	40.80	Wastani
10	Maandalizi ya Ufundishaji	1	15.9	15.90	Hafifu

